



Wanawake wanaofanya biashara ya kuchakata

Changamoto zinazowakabili wanawake katika biashara ya samaki

Wanawake wengi wanajaribu kujishughulisha ili kujipatia kipato, lakini wengi wao wanakabiliwa na changamoto zinazowakwamisha. Wanawake wanaojishughulisha na samaki nao wanakabiliwa na hali hiyo. Mara nyingi hawana rasilimali za kustawisha maisha yao. Wanapata ugumu katika kujenga mtaji. Njia kuu ambayo kwayo wanawake wameweza kujinyanyua kiustawi ni kwa kujiunga katika vikundi na kushirikiana.

Kuzikabili changamoto

Mfano mmoja mzuri ni wanawake wa Mwalo wa Kiyindi nchini Uganda ambao walijiunga na kuunda Umoja wa Wanawake Wachakata Samaki wa Kiyindi (KWFPA). Chama hiki kina wanachama 60, wengi wao wakiwa wanawake. Kikundi hiki kilisajiliwa rasmi mwaka 2010 baada ya kushiriki mafunzo kuhusu njia bora za kuhifadhi mazao baada ya kuvua na jinsi ya kuongeza thamani katika samaki. Waligundua kwamba wasingaliweza kuzishinda changamoto zilizowakabili kila mmoja peke yake. Changamoto hizo zinajumuisha kipato duni, kuhan-gaika na samaki wenye ubora duni, hali na njia zisizozingatia usafi wakati wa kuchakata, ukosefu wa teknolojia sahihi katika kuongeza ubora wa samaki na kukosa maarifa kuhusu namna ya kuongeza wateja wa samaki na muda wa kuwahifadhi.

Kushirikiana

Wanawake hawa waliunda chama na kuwachagua viongozi wao kidemokrasia. Kwa kuwa na uongozi mzuri, wanawake hawa wameweza kupiga hatua na kuzishinda changamoto kadhaa. Kushirikiana katika kikundi kunarahisisha kuvutia msaada kutoka katika miradi ya maendeleo na mashirika.

Kushirikiana kama kikundi, wanakausha samaki pamoja katika vichanga maalumu vilivyonyanyuliwa. Ubora ulioimarishwa wa samaki umewawezesha wanawake hawa kulenga masoko bora zaidi, huku wakiandaa na kujaribu bidhaa mpya za samaki. Wanawakaanga na kuwafungasha samaki ili watumike kama kitafunwa. Ubora wa samaki wao waliokaushwa ni mzuri kwa sababu wanatumia teknolojia bora zaidi. Hii imewasaidia kupata kipato kizuri kwa samaki wao na kuongeza kipato chao.

Kushiriki katika Vyama vya Kuweka Akiba na Kukopa vya Kijiji (VSLA) / Vyama vya Ushirika vya Akiba na Miko-po (SACCO)


Wanachama wote wanashiriki katika utaratibu wa kuweka akiba na kuko-pa. Manufaa ya kushiriki katika VSLA ni pamoja na kupata fedha nyakati za dharura na kuwawezesha hata wale wenye kipato kidogo kushirikiana na wenzao.

Tazama video

<https://youtu.be/9T5Xq7rp54M>



©FAO/Yaa Danso



Pitisha simu kwenye
alama hii ili kutazama
video

